Habari na Maoni

بسم الله الرحمن الرحيم

# Watawala wa Pakistan Wanataka Kulitambua Umbile la Kiyahudi (Imetafsiriwa)

**Habari:**

Mnamo tarehe 18 Oktoba, mkuu wa jeshi Asim Munir alithibitisha tena uungaji mkono usioyumba wa Pakistan kwa suluhisho la dola mbili kwa msingi wa mipaka ya kabla ya 1967, na Jerusalem kama mji mkuu wa Palestina huru. (Tribune)

**Maoni:**

Wakati Waziri Mkuu wa Pakistan alipoidhinisha mpango wa Trump kwa Gaza, Waislamu wa Pakistan walilaani msimamo wa utawala huo. Kisha mnamo tarehe 3 Oktoba 2025, Waziri wa Mambo ya Nje, Ishaq Dar, alisema, “Niliweka wazi kuwa hoja 20 ambazo Rais Trump aliziweka hadharani sio zetu. Mabadiliko yalifanyika kwenye rasimu yetu. Ninayo rekodi. Hata hivyo, haya ni matokeo ya mwisho, na hakuna nafasi ya siasa.” Kwa hivyo, utawala wa Munir-Sharif umekubali matokeo ya mwisho ambayo ni mpango wa Trump wa kusalimisha sehemu kubwa ya Ardhi Iliyobarikiwa ya Palestina kwa umbile la Kiyahudi.

Ama kuhusu “msimamo wake wa kimaadili,” utawala wa Munir-Sharif unaunga mkono suluhisho la dola mbili, ambapo sehemu kubwa ya Palestina imesalimishwa kwa umbile la Kiyahudi, ingawa Uislamu unakataa kabisa uvamizi wa Kiyahudi. Aidha, utawala wa Munir-Sharif unaunga mkono mpango wa Trump ambao unahakikisha usalama wa umbile la Kiyahudi, kwa kuondoa upinzani mjini Gaza, kwa kutumia Kikosi cha Kimataifa cha uwekaji Utulivu (ISF), ambacho kitajumuisha askari kutoka Jeshi la Pakistan.

Waislamu wa Pakistan wanajua kwamba utawala wa Munir-Sharif uko tayari kutambua umbile la Kiyahudi, mara tu Saudi Arabia itakapofanya hivyo, chini ya Makubaliano ya Abraham. Mnamo tarehe 17 Oktoba 2025, Rais wa Marekani, Donald J. Trump alisema, “Nataraji kuona Saudi Arabia ikiingia, na nataraji kuona wengine wakiingia. Nadhani Saudi Arabia itakapoingia, kila mtu ataingia.”

**Enyi Waislamu wa Pakistan!** Wanazuoni wa zamani walijua kwamba hakuna jambo lililo faradhi zaidi, baada ya Iman, kuliko kumzuia mtu ambaye amepora shubiri moja ya ardhi ya Kiislamu. Ibn Abidin anasema katika maelezo yake ya Hashiya (3/238), وفرض عين إن هجم العدو على ثغر من ثغور الإسلام فيصير فرض عين على من قرب منه، فأما من وراءهم ببعد من العدو فهو فرض كفاية إذا لم يحتج إليهم، فإن احتيج إليهم بأن عجز من كان بقرب العدو عن المقاومة مع العدو أو لم يعجزوا عنها ولكنهم تكاسلوا ولم يجاهدوا فإنه يفترض على من يليهم فرض عين كالصلاة والصوم لا يسعهم تركه، وثم وثم... إلى أن يفترض على جميع أهل الإسلام شرقاً وغرباً على هذا التدريج “Na ni faradhi kwa kila mtu binafsi (fard ayn) ikiwa adui atashambulia moja ya mipaka ya Uislamu basi inakuwa ni faradhi ya kila mtu binafsi kwa wale ambao wako karibu na adui, ama kwa wale walio nyuma yao, kwa masafa kutoka kwa adui, basi ni faradhi ya kutoshelezana (fard kifaya), ikiwa hawahitajiki. Ikiwa wanahitajika kwa sababu wale walio karibu na adui hawawezi kuwakimbiza adui huyo, au wanaweza kufanya hivyo ila ni wavivu na hawapigani, basi ni faradhi ya kila mtu mmoja mmoja kwa wale walio karibu nao. Ni sawa na faradhi ya mtu binafsi ya Swalah na Saumu, na hawawezi kutelekeza wajibu huo. Kisha faradhi ya kila mtu mmoja mmoja inaenea kwa wengine... Hadi iwe ni faradhi kwa Waislamu wote, mashariki na magharibi kwa utaratibu huu.”

Ni lazima tukatae jaribio lolote la kulitambua umbile la Kiyahudi. Ni lazima tuendelee na matakwa yetu ya kukusanywa majeshi ya Waislamu kwa ajili ya ukombozi wa Palestina na Al-Masjid Al-Aqsa.

**Enyi Wanajeshi wa Jeshi la Pakistan:** Kauli hizi za kudhalilisha zinazotolewa na maafisa, ambazo zinatambua uhalali wa umbile nyakuzi  na kuchukulia uwepo wake na usalama wake kuwa ni jambo la kawaida, hazitokani na Umma na wala haziuwakilishi. Badala yake, zinatolewa na tawala zilizonasibishwa na wakoloni, zinazoendeleza miradi yake na kufanya kazi ili kuilinda. Ummah ambao nyinyi ni miongoni mwao, na ambao ardhi na hadhi yake muliapa kuilinda, unalikataa kabisa umbile hili na kuliona kuwa ni adui mnyang'anyi ambaye si wa kuishi pamoja naye wala kufanya naye mapatano, bali ni wa kupigwa vita na kung'olewa.

Wajibu wenu wa Shariah leo ni kuhamasika kwa ajili ya kunusuru Dini yenu, Ummah wenu, na matukufu yenu, na kukataa utiifu wenu kwa watawala waliosalimu amri, na kuelekeza silaha zenu kwa adui wa kweli wa Ummah, ili muandike hadithi za historia ya ushindi kama walivyofanya babu zenu.

**[وَمَا لَكُمْ لَا تُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ وَالْوِلْدَانِ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْ هَذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ أَهْلُهَا]**

**"Na mna nini msipigane katika Njia ya Mwenyezi Mungu na ya wale wanao onewa, wanaume na wanawake na watoto, ambao husema: Mola Mlezi wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhaalimu!"** [Surah An-Nisaa: 75]

**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**
**Shahzad Shaikh – Wilayah Pakistan**